

Kikundi cha umri

10-15



Maambukizi  
ya

Magonjwa  
ya ngono



## Magonjwa yatokanayo na ngono ni nini?


STI au Maambukizi ya Magonjwa ya Ngono – ni maambukizi ya Magonjwa yanayoenezwa kwa kufanya ngono isiyo salama. Endapo utafanya ngono ya ukeni, mkunduni, au kwa kulamba sehemu za uke bila ya kutumia kinga[kondomu] uko hatarini kuambukizwa magonjwa yatokanayo na ngono (STIs). Magonjwa ambayo ni ya kawaida ni pamoja na UKIMWI, kisonono, malengelenge, kaswende, na gonorea.

Mtu yeyote anaweza kupata magonjwa yatokanayo na ngono, hata kama umefanya ngono mara moja. Si lazima uwe na washirika wengi ili upate magonjwa hayo.

## Nitaambujie kuwa nina STI?


Ni muhimu kujua viashiria vya magonjwa yale ya kawaida yatokanayo na ngono. Ukitambua moja ya viashiria vifuatavyo, ni vyema kwenda kituo cha afya ukapimwe, na utibiwe.

- ▲ Kutokwa na majimaji yasiyo ya kawaida, yenye rangi njano, au kijani mpauko, ukeni, au kwenye mboo (yaweza yakawa yanawasha, au kutoa harufu)
- ▲ Maumivu wakati wa kutoa mkojo
- ▲ Kujisikia kukojoa mara kwa mara



- ▲ Maumivu chini ya kitovu (kinena)
- ▲ Vidonda, vipele, malengelenge, uvimbe, kusunguka mboo, uke, au mkundu
- ▲ Kuwashwa, malengelenge, na maumivu (katika sehemu za siri)
- ▲ Uvimbe unaouma, kwenye uke, mapumbu na mboo.
- ▲ Maumivu wakati wa kufanya ngono
- ▲ Kutokwa damu wakati au baada ya kitendo cha ngono
- ▲ Hedhi zisizo na mpangilio
- ▲ Kwa wanawake, homa kali na viashiria vilivyotajwa na hasa maumivu makali chini ya kitovu, ni jambo baya sana

Huwezi kumtambua mtu mwenye magonjwa yatokanayo na ngono kwa kumtazama tu, kwa vile magonjwa mengine yatokanayo na ngono kama vile chlamydia hauna viashiria vya wazi. Kwa hiyo, wewe na mwenzi wako mnaweza mkawa na magonjwa yatokanayo na ngono bila kujitambua. Ndio maana ni muhimu kupimwa mara kwa mara ikiwa unafanya ngono bila ya kutumia kinga (kondomu).





Angalia  
kipeperushi  
cha “Hebu  
tutumie  
kondomu”.

## Ninawezaje kujikinga na STIs

- ✓ **Tumia kondomu kwa usahihi kila mara ufanyapo ngono.** Hi inakupunguzia hatari ya kupata, au kusambaza (STIs) magonjwa yatokanayo na ngono. Lakini endapo mwenza wako ana malengelenge, vipele au vidonda katika sehemu zake za siri ambavyo havijafunikwa na kondomu, basi utakuwa huna kinga.
- ✓ **Nenda ukapime mara kwa mara.** Hata kama umekuwa na mwenza wako kwa muda mrefu, ni vyema kwenda kupima, ili mradi muwe salama.
- ✓ **Usitegemee mitishamba.** Haitibu magonjwa yatokanayo na ngono. Na endapo unaishi na Virusi vya UKIMWI, itasitisha tiba yako kufanya kazi.




## Kwa nini nipimwe?

Usipopimwa, huwezi ukapatiwa tiba ya haraka. Magonjwa mengine ya STIs yasipopatiwa tiba kwa muda mrefu yanaweza kuathiri afya, na kukuletea maumivu makali sana. Magonjwa yatoanayo na ngono yasipotibiwa kwa muda mrefu, yanaweza kupelekea kutoweza kupata tena watoto. Na kuisha na STIs kunakuweka katika hatari zaidi ya kupata UKIMWI.

Habari njema ni kuwa STIs nyingi zinatibika kwa urahisi. Nyingine kama vile vidonda sehemu za siri, au UKIMWI, hayatibiki bali viashiria vinaweza kuelekea kwenye hali nzuri. Endapo vipimo vitaonesha uko na UKIMWI, bali unatumia dawa zako kama ipasavyo, ina maana una maisha bado mbele yako.

## Niende wapi kwa matibabu?

Unaweza ukawa na wasiwasi juu ya kwenda kupimwa. Lakini hakuna haja ya kuona haya. Unaweza kwenda katika kituo chochote cha afya karibu nawe kupimwa sehemu yoyote ambako una haki ya heshima na usiri.



Endapo una mwenza wako wa kila mara, unaweza kwenda naye kliniki, maana huenda wote mkahitaji kutibiwa. Endapo wewe pekee ndio umetibiwa, halafu wewe na mwenzi wako mnafanya ngono bila kinga, kuna uwezekano mkubwa wewe kupata tena maambukizi. Bali kama huna mwenza wa kila mara, ni vyema mshirika huyu wa sasa akapimwa pia.

Unafanya jambo jema: Kuwajibika juu ya afya yako, na afya ya wengine.

